**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OWM – TAMISEMI HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI SHULE YA SEKONDARI KIBITI**

Simu : +255 712617673
+255 788320321
+255 685141818

Barua pepe : kibitibss@gmail.com

S .L .P. 15
Kibiti
Tanzania

**KUMB.NA. ED/KSS/J.1/21**

…………………………………….

……………………………………. …………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE**

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha **TANO kwa mwaka wa masomo .................** katika shule ya Sekondari Kibiti katika Tahasusi ya Tunampongeza kwa mafanikio hayo.

Shule itafunguliwa tarehe **...................** na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe **.........................**

Shule ya Sekondari Kibiti ipo katika **Mkoa** wa **Pwani** umbali wa kilomita 134, Kutoka Dar-es-Salaam. Kwa wanafunzi wanaotoka Mikoa ya Kusini (Lindi na Mtwara) washuke kwenye lango la shule kilometa nne baada ya kupita mji mdogo wa Kibiti unapoelekea Dar –es-Salaam. Kwa wanafunzi wanaotoka mikoa mingine wafike **MBAGALA RANGI TATU – DSM,** ndipo watapata magari ya moja kwa moja kuelekea Kibiti au Ikwiriri, na washuke kituo kinachojulikana kwa jina la KINYANYA. Ndipo shule ilipo.

Mwanao atapokelewa shuleni endapo atasoma vyema maelelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo kwenye viambata vifuatavyo **A - G**

A. Maelezo Maalumu ya Kujiunga Na Shule
B. Michango mbalimbali ya shule.
C. Sheria,Kanuni na taratibu za shule
D. Fomu ya ya Afya (Mwanafunzi apimwe na ijazwe na Daktari aliyemhudumia)
E. Ahadi/Kiapo cha mwanafunzi.
F. Vitabu
G. Vifaa Vya usafi.

Ni matumaini yetu kwamba mwanao atasoma na kuzingatia maelekezo yote. Ni vyema Mzazi/Mlezi umtimizie mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.Kama kuna changamoto au maswali yoyote unaweza kupiga simu kwa namba zilizoainishwa hapo juu au kwa kutumia barua pepe ya shule.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIBITI
S. L. P 15
KIBITI

MWAKYOMA .L.A
MKUU WA SHULE

## A. MAELEZO MAALUMU YA KUJIUNGA NA SHULE

1 **SARE**

**I. SARE YA SHULE**

a. Suruali mbili Dark bluu , za Darasani
b. Suruali mbili nyeusi za kushindia/shamba dress
c. Shati nyeupe mbili mikono mifupi zenye nembo ya shule
d. T-shirt mbili rangi ya njano yenye kola zenye nembo ya shule

NB **Sare hizi za shule zinapatikana shuleni kwa atakaye hitaji. Kwa wale watakao shona wao wenyewe, suruali iwe na upana wa chini inchi 16, marinda mawili pamoja na turn up.**

**II.MAHITAJI MENGINE:**

a. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vya kufunika visiwe na visigino virefu (Jozi 2)
b. Mkanda mmoja mweusi upana $1\frac{1}{4}$inchi usiwe na urembo wa aina yoyote
c. Soksi jozi 2 au zaidi nyeusi.
d. Viatu vya michezo.
e. Kandambili kwa ajili ya kuogea tu.
f. Sweta moja la **Dark Bluu** lenye shepu ya V.
g. Kila mwanafunzi lazima aje na Tracksuti ya blue bahari ambayo ataivaa siku za mwisho wa wiki.
h. Kila mwanafunzi lazima funguliwe akaunti Benki NMB au CRDB kwa ajili ya kuhifadhia fedha zake za matumizi. Kwa atakaye shindwa kufungua akaunti akiwa nyumbani atafungulia hapa hapa shuleni.

2. **MAHITAJI YA BWENI**

i. Godoro la nchi $2\frac{1}{2}$ kwa 6
ii. Shuka rangi ya sky blue Jozi mbili iii. Mto na foronya 2 za sky blue
iv. Taulo
V Nguo za ndani (za kutosha),Vest nyeupe zisizo na urembo na mashine za kunyolea ndevu
vi. Ndoo mbili kubwa zenye mifuniko lita 20
vii. Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili
viii. Vyombo vya chakula, Sahani, Bakuli,Kikombe, Kijiko, Chupa ya chai anaweza kuja na ‘’**HOT POT**’’ 1 ndogo kwa ajili ya dharura za kiafya.
ix. Chandarua futi 3x6. Ya pembe nne.Pia kia mwanafunzi lazima aje na dawa ya mbu ya kujipaka kwa ajili ya kujilinda na mbu wanaosambaza Malaria.

3. **MAHITAJI YA TAALUMA**

a) Rimu 2 kwa mwaka A4 aina ya pekee
b) Madaftari 06 (Counter Book) ,Kalamu/Penseli za kutosha Mkebe wa hisabati (Mathematical Set)
c) Kwa mwanafunzi wa CBA, na PCB alete **dissection kit** kwa ajili ya kujifunzia

d) Scientific Calculator kwa wanafunzi wa CBA, PCB, PGM, HGE,HGK,HGL, PCM, PMC's na EGM. (**CASIO fx- 991 MS 2nd edition**)

e) Faili 2 kwa ajili ya kuhifazia mitihani na kumbukumbu zingine ''**Folder file**''

f) Graph pad moja kwa wanafunzi wa CBA, PCB, PCM, PGM, EGM, PMC's na HGE

g) kwa wanafunzi wa sayansi **CBA, PCB, PCM,PMC's** na **PGM** wanatakiwa kuwa na koti la maabara (**lab coat)** kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

**NB:Ili kuepusha usumbufu na gharama ya usafiri unashauriwa vitu kama Godoro,chandarua,ndoo,Rimu,vifaa vya usafi,vitabu,scientific Calculator, Lab coat, Truct suit,Dissection Kit,vyombo vya chakula n.k kununua katika duka la shule kwa atakaye hitaji.**

## B. MICHANGO MBALIMBALI:

### JEDWALI LA MICHANGO MBALI MBALI

| S/N | MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Kuendesha shule | 65,000/= |
| 4 | Kitambulisho | 5,000/= |
| 5 | Tahadhari | 5,000/= |
| 6 | Nembo | 5,000/= |
| **7** | **JUMLA KUU** | **80,000/=** |

Michango yote ilipwe kwenye Akaunti Namba **21301100034 NMB**
Jina la Akaunti ya shule ni **Kibiti Reccurent Expenditure** Utapata huduma katika tawi lolote la Benki ya NMB Tanzania.Jina la mwekaji liwe la mwanafunzi na si mzazi/mlezi.Mwanafunzi aje na **PAY INSLIP** ya benki wakati wa kuripoti shuleni, **kamwe hatutapokea pesa mkononi.**

## C: SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule ya sekondari Kibiti inaamini kuwa hakuna mafanikio ya kitaaluma bila nidhamu, hivyo Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya **HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII, USAFI na TABIA NJEMA** kwa ujumla

Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri Kwa heshima na tabia, kauli na vitendo hivyo:

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri
2. Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu na ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.
3. Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi
   (a) Kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya.
   (b) Kufuga kucha na nywele
   (c) Kufuga ndevu
   (d) Kunyoa kipara
   (e) Kumpiga mwenzake
   (f) Kutukana
   (g) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
   (h) Kuvaa vitu kama mapambo mfano Heleni, Mikufu bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali, Kofia, Kanzu, Vilemba, Suruali fupi Kwa kuwa Shule hii ni ya **Serikali**. (i) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu
   (j) Kuvaa kaptura na kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule
   (k) Kuvaa suruali chini ya kiuno
   (l) Kuvaa nguo za mtindo, mfano- model
4. Mwanafunzi atasimama kwenye mstari wakati wa kupata huduma
5. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali
6. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu Kwa wengine anapokuwa Darasani, Maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prepo) na katika mikusanyiko yoyote mfano paredi nk
7. Mwanafunzi LAZIMA awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.Hivyo Mwanafunzi:-
   A. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
   B. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa
   C. Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa
   D. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call). Ukaguzi wa Usafi , kupandisha Bendera ya Taifa, Mikutano ya nyumba (MABWENI), Mikutano ya darasa na Mabaraza ya shule.
   E. kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalio ya Alasiri (9;00-11:00), usiku kuanzia saa 01:30-5;00 pamoja na alfajili 10:45-12:00
   E.Siku ya Jumamosi maandalio ya masomo yataanza saa 4 asubuhi hadi saa 7 mchana
8. Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na **KITAMBULISHO** kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule.
9. Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, anapaswa kuwa na kibali (Pass) cha maandishi.(Kilichotolewa na Mkuu wa shule au Mwalimu wa Zamu)

11`. Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia chakula bwenini, wala kutumia **electrical heater** au jiko la aina yoyote

12. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhutasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule.
13. USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi Kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.
14. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za shule ya sekondari Kibiti muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati au T shirt yake. **Mavazi ya nyumbani Hayaruhusiwi kabisa.**
15. Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki simu au sehemu ya simu **kama laini, Charger, earphone, Ipadi nk.**
16. Hairuhusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.
17. **MAENEO YASIYORUHUSIWA**:

    **Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila sababu maalumu**

    - Ofisi za shule
    - Chumba cha wafanyakazi
    - Maabara
    - Jikoni
    - Nyumba za wafanyakazi
    - Nyumba za ibada

    **Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea maeneo yafuatayo**

    - Vilabu vya pombe
    - Majumba ya starehe
    - Majumba ya kufikia wageni
18. **BWENINI**
    - Kila mwanafunzi atawajibika kufanya usafi wa kila siku katika eneo atakalopangiwa na kiongozi wake
    - Mwanafunzi lazima awepo bwenini kwenye ukaguzi kila siku ya jumatano asubuhi.
    - Mwanafunzi haruhusiwi kumkaribisha mgeni yeyote bwenini wakati wote. Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali aliyokabidhiwa bwenini
    - Ni marufuku kupeleka viti ,meza na chakula Bwenini.

**<u>MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI AU KUSIMAMISHWA SHULE:</u>**

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga na ulawiti.
3. Ulevi wa aina yoyote.
4. Utumiaji wa madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi,Cocaine ,Mirungi,Kubeli nk. 5. Uvutaji wa sigara au Bangi
6. Makosa ya jinai
7. Kuoa au kuolewa
8. Kuharibu Kwa makusudi Mali ya umma.
9. Kupigana au kumpiga mwingine.
10. Kudharau Bendera ya Taifa
11. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule
12. Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma Kwa namna yoyote(
13. Kutoa lugha ya matusi
14. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla
15. Kutohudhuria vipindi
16. Ubakaji.
17. Kuwa na simu ya mkononi. (KUMILIKI AU KUTUMIA SIMU YA MKONONI)

**MAMBO MENGINE YA MUHIMU ANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

- Medical examination fomu ambayo itajazwa na mganga wa Hospitali ya Serikali mara tu atakapowasili shuleni na kuikabidhi.
- Fomu ya Melezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo ,fujo na makosa ya jinai
- Fomu ya mzazi kukiri kukubalina na sheria ,kanuni na maelezo mengine na shule.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OWM – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI SHULE YA SEKONDARI KIBITI**

Simu: +255 712617673
+255 788320321
+255 685141818
Barua pepe : kibitibss@gmail.com

S .L .P. 15
Kibiti
Tanzania

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

**MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi……………………….……………………………..Adm. NO……………
2. Kidato …………………mchepuo……..………..mwaka………………
3. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………….
4. Kabila la mwanafunzi……………………………………………………………
5. Uraia wa mwanafunzi………………………………………………………………………
6. Tarehe ya kujiunga na shule ya sekondari ya Kibiti………………………………..
7. Shule aliyotoka ya sekondari……………………………………………………………
8. Masomo utakayokuja kusoma………………………………………………………………
9. Kama ni mlemavu,taja aina ya ulemavu………………………………………………………
10. Je unarudia kidato?……….kwa nini?.........................................................................................
11. Dini ya mwanafunzi…………………………………Dhehebu……………………………………………
12. Anwani ya kudumu ya mwanafunzi S.L.P………………………………………………………...

Wilaya…………………………………………….Mkoa……………………………………………..
Tarafa……………………………………………Kata………………………………………………..

Kijiji/Mtaa…………………………………………………Namba ya nyumba……………
Simu ya nyumbani………………………………………………………………………
Simu ya ofisini……………………………………………………………………

**BABA**

13. Jina la Baba…………………………………………………………………….
14. Je,yu hai ?……………………………………………………………………………………..
15. Kabila la baba……………………………………………………………………………………
16. Anwani yake ya sasa…………………………………………………………………………….
17. Kazi yake………………………………………………………………………………………
18. Mwajiri wake…………………………………………………………………………………
19. Dini ya baba …………………………………..dhehebu…………………………………………
20. Je,baba na mama wanaishi pamoja?.........................................................................................
21. Simu ya baba………………………………………Ya kazini……………………………………

**MAMA**

22. Jina la mama…………………………………………………………………………………..
23. Je,yu hai?.........................................................................................................................
24. Kabila la mama……………………………………………………………………………….
25. Mwajiri wake ………………………………………………………………………………...
26. Anwani yake ya sasa………………………………………………………………………….
27. Dini ya mama………………………………………Dhehebu… .................................................. 28. Kazi yake …………………………………mwajili wake……………………………………
29. Simu ya nyumbani……………………… ….Ya ofisini……………………………………..

**MLEZI**

30. Jina la mlezi……………………………………………………………………………………
31. Kabila la mlezi…………………………………………………………………………………….
32. Uhusiano na mwanafunzi ukoje?.......................................................................................................
33. Anwani ya sasa……………………………………………………………………………………
34. Kazi yake………………………………………………………………………………………….
35. Mwajiri wake……………………………………………………………………………………..
36. Dini ya mlezi……………………………………Dhehebu……………………………………
37. Simu ya nyumbani…………………………………………..Ya kazini……………………………

**NDUGU WENGINE**

| JINA | ANWANI | SIMU | UHUSIANO |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**PICHA ZA NDUGU WENGINE**

TAARIFA NYINGINEZO KAMA ZIPO

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

Sahihi ya mwanafunzi……………………………………….Tarehe…………………………………….

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OWM – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI SHULE YA SEKONDARI KIBITI**

Simu: +255 712617673
+255 788320321
+255 685141818
Barua pepe : kibitibss@gmail.com

S .L .P.
Kibiti
Tanzania

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART 'A'**

FROM……………………….
……………………………….
……………………………….

TO THE MEDICAL OFFICER
………………………………...
………………………………...

Mr./Miss ........................................................................................................... (Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full – time student. The examination should include the following categories (I – III) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of a defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl student ineligible for studies.

I (a) Eyesight (e) Venereal Diseases
(b) Hearing (f) Leprosy
(c) Speech (g) Epilepsy
(d) Limbs
II Neuroses
III Other serious diseases

Date………………………………………… Signature……………………………………

**PART B:**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above – named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full – time student.

I (a) Eyesight…………………… (e) Venereal Diseases ............................
(b) Hearing................................ (f) Leprosy ...................................
(c) Speech................................... (g) Epilepsy …………………...
(d) Limbs.........................................
II Neuroses…………………………………………………………………….................
III Other serious diseases…………………………………………………………………

Date……………………………………………Signature…………………………….........
Station……………………………………... Designation………………………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OWM – TAMISEMI HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI SHULE YA SEKONDARI KIBITI**

Simu : +255 712617673
+255 788320321
+255 685141818
Barua pepe : kibitibss@gmail.com

S .L .P.15
Kibiti, Tanzania

---

## E. AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi …………………………………………………………………………………………………………

Ambaye nimechaguliwa kujiunga na SHULE YA SEKONDARI KIBITI KIDATO CHA TANO Mchepuo wa ….................................. mwaka wa masomo ............. ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii ili kufikia malengo yaTaifa na Shule ya Sekondari ya Wavulana Kibiti.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni:

i. Nitasoma Kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo niliyo changuliwa kusoma
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
iv. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/ mlezi wangu.......................................................................................... (Jina la mzazi) Kwa ajili ya hatua zaidi.

Saini ya mwanafunzi …………………………………… Tarehe ………………………………………………………

---

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ........................................................................................................ninakubali mtoto wangu
…........................................................................................Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari kibiti mwaka 2026. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.
Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule katika kusimamia nidhamu ya mwanangu na wakati wote nitahakikisha kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa.

Anuani yangu ya kudumu ni ………………………………………………………………..
………………………………………………………………….
Simu ………………………………………………………..

Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nilazimika kuujulisha uongozi wa shule kwa maandishi

Saini ya Mazazi/Mlezi ……………………………………….Tarehe ………………………….

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIBITI
S. L. P 15
KIBITI

MWAKYOMA .L.A
MKUU WA SHULE

## F. VITABU

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na baadhi ya vitabu kutokana na masomo (Mchepuo) anayokuja kusoma hapa shuleni.Mwanafunzi atakaguliwa vitabu hivi mara tu atakapofika shuleni.(NB Unaweza kuvipata Duka la shule)

**1. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

Kila mwanafunzi **lazima** aje na kitabu cha somo la Historia ya tanzania na maadili. By TIE

**2. BASIC APPLIED MATHEMATICS**

Kila mwanafunzi aliechaguliwa kusoma michepuo ya CBA, PCB, na HG.E anatakiwa kuja na kitabu cha Basic Applied Mathematics By TIE

**3. ECONOMICS**

Kila mwanafunzi anaekuja kusoma somo la Economics anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya

- Modern Economics By Robert Mudida
- Principle of Economics By M.L.Jinghan
- Microeconomics book for Advanced secondary school form five By TIE
- Economics Simplified By N.A.Saleem

**4. BIOLOGY**

Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kusoma somo la Biology anatakiwa kuja angalau na Vitabu viwili kati ya

- Biological Science By D.J Taylor
- Biology for Advanced level secondary school form five By TIE
- Understanding Biology for Advanced level By Grenn & Susan Toole
- Biology a functional approach 4th Edition By M.B.V.Roberts
- Modern ABC Biology class XII Part I & II By Dr.B.B.ARORA.
- S. CHAND'S Biology for class XI & XII By Dr.P.S.VERMA

**5. CHEMISTRY**

Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kusoma somo la Chemistry anatakiwa kuja na vitabu angalau viwili kati ya

- Modern chemistry ABC of Class XI Party I & II By Dr .S.P.Jauhar
- Physical Chemistry By Chand
- Physical chemistry for Advanced level secondary schools
- General chemistry for Advanced level secondary schools
- Organic chemistry for Advanced level secondary schools
- Inorganic chemistry for Advanced level secondary schools

**6. GEOGRAPHY**

Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kusoma somo la Geography anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya

- Physical Geography for Advanced secondary school By TIE
- Practical Geography for Advanced secondary school By TIE
- Human Geography for Advanced secondary school By TIE
- Fundamental Geography By Josephat Mwita

**7. ADVANCED MATHEMATICS**

Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kusoma somo la Advanced Mathematics anatakiwa kuja na vitabu angalau viwili kati ya

- Advanced mathematics form five By S.I.Sillem
- Advanced mathematics for advanced secondary school forrm five and six By TIE
- Advanced mathematics form five and siv By Mayombya

**8. AGRICULTURE**

Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kuja kusoma somo la Kilimo anatakiwa kuja na vitabu vifuatavyo

- Agriculture for Advanced secondary school form five By TIE
- East African Agriculture By Ngugi
- Introductory Soil Science A.P Urio et all
- Farm equipment,Machinery,Structure and Buildings By L.Anyonzo
- Lonhorn secondary Agriculture (2005) By J.mailu & D.Mwangi (I-IV)

**9. PHYSICS**

Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kusoma somo la Physics anatakiwa kuja na vitabu angalau viwili kati ya

- Physics for Advanced secondary schools form five By TIE
- Physics for advanced secondary schools form six By TIE
- Modern ABC of Physics Part II By Satish Gupta
- Modern ABC of Physics Part I By Satish Gupta
- S.Chand's Principles of Physics for Class XI By V.K.Mehta & Rohit Mehta
- S.Chand's Principles of Physics for Class XII By V.K Mehta & Rohit Mehta

**10. COMPUTER SCIENCE**

Kila mwanafunzi anayekuja kusoma somo la Computer Science anatakiwa kuja na vitabu japo viwili kati ya

- Computer Science for Advanced secondary schools form five By TIE
- Computer Science for Advanced secondary schools form six By TIE
- Understanding Computer Science for Advanced Level by Ray Bradley
- Advanced level Computer Science Coursebook by Cambridge IAS

**11. HISTORY**

Kila mwanafunzi anayekuja kusoma somo la History anatakiwa kuja na vitabu japo viwili kati ya

- History for Advanced secondary schools form five By TIE
- History for Advanced secondary schools form six By TIE
- Advanced level History nem curriculum By Pascrates Fidelis Rutta

**12. ENGLISH LANGUAGE**

Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kuja kusoma somo English Language anatakiwa kuja na vitabu viwili kati ya

- Advanced English Oxford Dictionary 7th Edition (**Lazima aje nayo**)
- Advanced level English language (Structure & stylistics) By N.Asheli
- Contemporary English for Advanced level By Francis Myawi
- English language One Form five & six By Kadeghe M

NB;mwanafunzi anatakiwa pia kuja na angalau vitabu viwili vya **PLAY**,vitabu na vitabu Viwili vya **NOVELS**

**NOVELS**

- Animal Farm (George Orwel)
- The opportunitist Elite (nyambali nyangwine)
- The horizon unveiled ( forewells mwaisela)
- Chasing the leopard finding the lion ( julie wakemaa)

**PLAY**

- A teste of heaven (F.M.Topan)
- The government inspector ( Nicolai Gogo))
- An enemy of the people (Henrick Ibsen)

**POEMS**

- The Summons By Charles Mloka
- The Lament Of The Silent By Jared Angira

**13. KISWAHILI**

Kila mwanafunzi aliyepangwa kuja kusoma somo la Kiswahili anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya

- Samakisa na Samikisa ( Masamba na wenzake)
- Kiswahili kidato cha tano na sita (Oxford)
- Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili 2 (Nyambari Nyangwine)
- Tafsiri na Ukalimani (Mwansoko)
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI) **Lazima aje nayo**

Vile vile mwanafunzi anayesoma Kiswahili anapaswa kuja na vitabu vya **RIWAYA** viwili**,MASHAIRI** viwili na **TAMTHLIYA** viwili (**Chagua hapo chini kwenye orodha)**

**USHAIRI**

- Fumbo linaloelea ( Nyambali Nyangwine)
- Malenga wa ziwa kuu (wallah bin wallah)
- Andamo,msafiri,safarini (mohammed k.ghassani)
- Wosia wa baba (ahmed m.amanzy)

**RIWAYA**

- Dunia uwanja wa fujo (euphrase kezilahabi)
- Ua la faraja (W.E.Mkufya)

- Mirathi hatari ( C.G.Mung'ongo)
- Wasifu wa siti binti saad (Shaban Robert)

**TAMTHILIYA**

. Mkwawa wa uhehe (M.M.Mlokozi)
. Shujaa mirambo ( Emmanuel Mbogo)
. usaliti mjini (Francis Imbuga)

**14.ACADEMIC COMMUNICATION**

Kila mwanafunzi **lazima** aje na kitabu cha somo la Academic Communication. By TIE

**E. VIFAA VYA USAFI**

Kila mwanafunzi ataleta kifaa kama ilivyoainishwa katika Jedwali hapa chini

| CBA | PCB | PCM | PGM | EGM | HG. E | HGK | HGL | HKL | PMCs |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| -Panga<br><br>-Watering cane<br><br>-Fagio la chelewa lenye mpini | -Fagio la kudekia lenye mpini (Squezzer)<br><br>- Fyekeo lilinolewa<br><br>-Fagio la chelewa lenye mpini<br><br>-Jembe lenye mpini | -Fagio la chelewa lenye mpini<br><br>-Mfagio laini wa sakafu<br><br>-Fyekeo lililonolewa<br><br>-Jembe lenye Mpini | -Fagio la kudekia lenye Mpini(Squezzer)<br><br>-Spade (chepe)lenye mpini wa chuma.<br><br>-Fagio la chelewa lenye mpini<br><br>-Brush la chooni | -Fagio la chelewa lenye mpini<br><br>-Jembe lenye mpini<br><br>-Fagio laini la sakafu lenye mpini<br><br>-Fagio la kudekia lenye mpini(squezzer) | -Fagio la chelewa lenye mpini<br><br>-mfagio mgumu wa sakafu<br><br>-Fagio lakudekia lenye mpini (squezzer)<br><br>-Jembe lenye mpini | -Reki yenye mpini<br><br>- Fagio la kudekia lenye mpini (Squezzer)<br><br>-Fagio la buibui lenye mpini | -Fagio gumu la sakafu (hard broom)<br><br>-Fagio la chelewa lenye mpini<br><br>-Mopper ya kudekia yenye Kindoo | -Jembe lenye Mpini<br><br>-Fyekeo lililonole wa<br><br>-Fagio la chelewa lenye mpini<br><br>-Fagio la kudekia lenye mpini(squezzer) | -Spade (chepe)lenye mpini<br><br>- fagio la buibui<br><br>-Brush ya chooni<br><br>-Fagio la chelewa lenye mpini. |